



MAONESHU YA MIAKA 60 YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR



Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimeshiriki kikamilifu katika maonesho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika kuanzia tarehe 8 hadi 19 Januari 2024 katika viwanja vya Fumba, Zanzibar.

Maonesho hayo yalikuwa ni sehemu muhimu ya kusherehekea miaka 60 tangu kufanyika kwa Mapinduzi ya Zanzibar ambayo yalikuwa na athari kubwa katika historia na mustakabali wa Zanzibar. Tukio hili la kihistoria lilikuwa na umuhimu mkubwa kwa Zanzibar na kwa watu wake, na kulenga kuenzi na kutafakari matukio ya zamani na maendeleo yaliyopatikana.

Katika banda la maonesho la Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, kulikuwa na wageni waalikwa mashuhuri waliojitokeza kutembelea na kujionea mchango wa chuo katika sekta ya usafirishaji. Miongoni mwa wageni hao walikuwepo Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Profesa Godius Kayharara, Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi la Chuo, Profesa Ulingeta Mbamba, na Kaimu Mkuu wa Chuo, Dkt. Zainabu Mshana.



Kaimu mkuu wa Chuo Dkt. Zainabu Mshana akitoa huduma kwa wananchi aliyefika katika banda la Chuo.

Viongozi hawa walitoa pongezi na kuthamini mchango mkubwa wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji katika kuendeleza sekta ya usafirishaji nchini. Walivutiwa na matunda ya elimu na mafunzo yanayotolewa na Chuo kujifunza zaidi kuhusu programu na kozi zinazotolewa na chuo.

Wakati wa ziara yao, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Profesa Kayharara, aliwashauri wanafunzi kuendelea kuwa

wabunifu na kujifunza teknolojia mpya zinazoendelea katika sekta ya usafirishaji. Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi la Chuo, Profesa Ulingeta Mbamba, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya chuo na sekta ya usafirishaji katika kuwezesha maendeleo endelevu. Kaimu Mkuu wa Chuo, Dkt. Zainabu Mshana, aliahidi kuendelea kuweka jitihada katika kutoa elimu bora na kukuza uwezo wa wanafunzi katika sekta ya usafirishaji.

Ushiriki wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji katika maonesho haya ulitia nguvu kubwa katika kuendeleza na kuonyesha mchango wa chuo katika kukuza sekta ya usafirishaji nchini. Pia ilikuwa ni fursa nzuri kwa viongozi na wageni waalikwa kuona juhudi na mafanikio ya Chuo katika kutoa elimu ya usafirishaji na kuandaa wataalamu wenye ujuzi.



Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa Chuo Prof. Ulingeta Mbamba akimsikiliza Kaimu Mkuu wa Chuo (katikati) katika Banda la chuo katika maonesho ambayo ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar

MATUKIO KATIKA PICHA



Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi Prof. Godius Kyharara (wa kwanza kulia) akipata maelezo kutoka kwa Kaimu Mkuu wa Chuo Dkt. Zainabu Mshana (mwenye kilemba cha bluu) alipotembelea banda la maonesho ya kilele cha mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika katika viwanja vya Fumba kuanzia tarehe 8-20 Januari 2024.



Watumishi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) wakiongozwa na Afisa Uhusiano Mkuu wa Chuo (NIT) Tulizo Chusi wakiwa kwenye picha ya pamoja katika Banda la chuo hicho kwenye Maonesho ya Biashara ikiwa ni Maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar yanayofanyika katika viwanja vya Fumba.